**JINA: ………………………………………………………………………………………………**

**NAMBA YA USAJILI: ………………………………………………………………………......**

**MKONDO: …………………………………………………………………………………...**

**KISWAHILI**

**KIDATO CHA KWANZA**

**AGOSTI 2022**

**SAA: 2**

**Hati ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari**

Maagizo

a) Andika jina lako, na nambari yako ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Andika mkondo wa kidato chako na tarehe
c) Jibu maswali yote
d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika karatasi hii.

**<u>Kwa matumizi ya mtahini pekee</u>**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 45 | |
| JUMLA | 60 | |

**UFAHAMU**

**SOMA TAARIFAIFUATAYOKISHA UJIBU MASWALI YOTE (ALAMA 15)**

Nilipojiunga na shule ya upili, nilisajiliwa katika chama cha Wapenda Mazingira. Chama hicho kilitunza na ***kuimarisha*** mazingira shuleni na hata ***viungani*** mwake. Wanachama walipenda sana kutunza njiwa, shore kishungi na shomoro, ndege walio na rangi na maombile ya kuvutia.

Walihifadhi kitalu katika pembe moja ya uwanja wa shule ambapo ungewaona nyuki wakifurahia maua. Vipepeo na buibui wa aina mbalimbali wangepatikana hapo. Aidha, usingewakosa chozi, ndege wapendao asali ya maua. Walifuga wanyama kama sungura, nguruwe na farasi.

Mwalimu mkuu, Bwana Hekima, alipendezwa na bidii hiyo na akaahidi kutupeleka sisi wanachama ***kutalii*** sehemu ya mbuga ya hifadhi ya Nakuru. Kweli,mchezo kwao hutuzwa.

Safari ilichukua wanafunzi hamsini na wawili. Njiani tuliona kobe aliyekua akivuka barabara. Dereva akasimamisha basi nasi tukashuka kuajabia maumbile yake. Kobe hakuonyesha kuadhirika.alifululiza akatokomea kichakani. Tukaondoka.

Tuliwasili lango kuu la hifadhi hilo yapata saa sita mchana. Tukapewa kiongozi wa safari. Ghafla bin vuu,nilisikia wenzangu wakimaka, “Mtazame… yaani ni mkubwa hivi!” nilipotazama nje kupitia dirisha la basi, nilimwona kifaru aliyetulia chini ya mti. Kado yake alipita ngiri kwa kasi huku ameinua mkia wake. Meno yake mawili yaliyotokeza kila moja kando ya kinywa yalimfanya aonekane wa kutisha. Alielekea kidimbwini ambamo viboko wawili walikua wakifurahia maji. Nilikubali kuwa, kutembea kwingi, kuona mengi.

Tulipokuwa tukila chakula chakula cha mchana ndani ya basi, alikuja nyani mkubwa karibu nasi. Alionekana kupendezwa na kuwepo kwetu pale.

Tuliendelea na safari hadi sehemu iitwayo Makalia. Maanguko ya jamii ya Makalia yalitustaajabisha. Hatua chache kutoka tulipokuwa tumesimama tulionambuni. Miongoni mwa ndege wote tuliowaona, waliokuwa wengi ni heroe. Walionekana ***wakitarazaki*** majini. Mwalimu wetu wa jiografia alitueleza mengi kuhusu ndege hao.

Kiongozi wa safari alitueleza kuwa sehemu ile ya Makalia ilisifika kwa sababu wanyama mbalimbali walifika pale kuzima kiu yao. Pia, weupe wa maji yakigonga kwenye magenge ni jambolililovutia wengi. Sisi hatukuwa na bahati nzuri kwa kuwa tulifika hapo wakati ambao wanyama wengi walikuwa tayari wameondoka kurudi malishoni.

Saa kumi na moja jioni tulikuwa hoi. Tulifurahia safari hiyo na kuwasimulia wenzetu shuleni kwa fasili. Baada ya majuma manne idadi ya wanachama iliongezeka.

**MASWALI**

1. Kwa nini wanafunzi walikwenda kuzuru mbuga ya wanyama? (ala2)

   .....................................................................................................................................

   .....................................................................................................................................

2. Ni mambo yapi yaliwastajabisha wanafunzi katika sehemu ya Makalia? (ala3)

   .....................................................................................................................................

   .....................................................................................................................................

   .....................................................................................................................................

3. Taja majukumu mawili ya chama cha mazingira shuleni. (ala2)

   .....................................................................................................................................

   .....................................................................................................................................

4. Safari hii ilikuwa na manufaa yapi kwa wanafunzi? (ala2)

   .....................................................................................................................................

   .....................................................................................................................................

5. Kwa nini idadi ya wanachama wa mazingira iliongezeka baada ya majuma manne?(ala2)

   .....................................................................................................................................

   .....................................................................................................................................

6. Taja methali moja iliyotumika kwenye Makala. (ala1)

   .....................................................................................................................................

7. Eleza maana ya maneno haya kama walivyotumika kwenye kifungu (ala3)

   (a) Kuimarisha

   .....................................................................................................................................

   (b) Akatokomea

   .....................................................................................................................................

   (c) Kutalii

   .....................................................................................................................................

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA )**

a) Eleza maana ya lugha (ala2)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

b) Taja sifa tatu za lugha (ala3)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

c) Eleza dhima tatu za lugha (ala6)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

d) Sauti ni nini? (ala2)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

e) Taja aina mbili za sauti (ala2)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

f) Eleza tofauti iliyopo kati ya aina mbili za sauti ulizotaja hapo juu. (ala2)

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

g) Andika sauti zenye sifa zifuatazo (ala4)

(i) Nazali kaa kaa laini

.....................................................................................................................

(ii) Kikwamizo ghuna cha mdomo na meno

.....................................................................................................................

(iii) Irabu ya nyuma wastani (kati)

.....................................................................................................................

(iv) Kiyeyusho cha kaakaa gumo

.............................................................................................................................

h) Fafanua maana ya silabu (ala2)

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

i) Bainisha silabi neno! (ala4)

(a) Wanyweshavyo

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

(b) Mbweha

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

(c) Ua

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

j) Andika neno lenye muundo ufuatao (ala2)

Irabu + konsonati + konsonanti + irabu

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

k) Eleza dhana ya sauti mwambatano (ala2)

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

l) Tofautisha maana katika sentensi hizi (ala3)

(i) Kazi imekwisha.

.............................................................................................................................

(ii) Kazi imekwisha?

.............................................................................................................................

(iii) Kazi imekwisha!

.............................................................................................................................

m) Weka shadda kwenye neno barabara kutoa maana mbili tofauti (ala2)

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

n) Bainisha maneno katika tungo zifuatazo (ala4)

(i) Nyanya hunipikia uji wa wimbi

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

(ii) Watoto wanachezea mpira

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

o) Onyesha aina mbili za viambishi katika neno lifuatalo (ala2)

Waliomtembelea.

.................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................

p) Fafanua aina zifuatazo za maneno (ala3)

(i) Nomino

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

(ii) Vitenzi

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

(iii) Vihisishi

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

**MWISHO**